*Mhtasari umeandaliwa naInternational Resource Group, Washington, DC na*
*Taasisi ya Kutathimini Rasilimali Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania*

# KUKUA KWA UTALII NA CHANGAMOTO ZA MAENDELEO KISIWA CHA MAFIA

## UTANGULIZI

Aliyekuwa Rais wa Marekani Bwana George W. Bush na Rais wa Tanzania Jakaya Kikwete walitiliana saini makubaliano ya kutekeleza Mpango wa Changamoto za Milenia utakaogharimu Dola za Kimarekani milioni 698.1. Lengo kuu la Mpango huu ni kupunguza umasikini kwa kuongeza ukuaji wa uchumi, kuongeza kipato ngazi ya kaya, na kupandisha ubora wa maisha kupitia uwekezaji katika miundombinu mbalimbali. Miradi itakayozingatiwa katika makubaliano haya ni pamoja na ujenzi wa uwanja vya ndege na barabara, upatikanaji wa nishati (umeme)) na usambazaji wa maji safi na salama. Miradi hii inatarajiwa iwasaidie Watanzania kupata nishati bora, usafiri mzuri na maji safi na salama ambavyo vitainua ubora wa maisha yao.

Uboreshaji wa uwanja wa ndege wa Mafia ni moja kati ya miradi ya miundombinu chini ya makubaliano haya. Njia pekee ya usafiri kufika Mafia imekuwa kwa vyombo vya majini na kwa watu wachache kupitia ndege. Hali duni ya uwanja wa ndege, viwango duni vya usafiri wa majini na kukosekana kwa bandari kumefanya usafiri kwenda Mafia kuwa mgumu na wa hatari sana. Kukosekana kwa njia bora za usafiri kumekwamisha harakati za maendeleo ya Mafia.

Madhumuni ya utengenezaji wa uwanja wa ndege wa Mafia ni kuboresha sehemu ya kutua ndege, kuegesha ndege, kuimarisha mipaka ya uwanja wa ndege, kuboresha kitengo za zima moto cha uwanja wa ndege, kuboresha jengo la kuteremkia na kuondokea abiria, kuweka maji na njia za mawasiliano zilizo bora zaidi. Kupitia uboreshaji huu, inatarajiwa kuwa usalama na ulinzi wa uwanja wa ndege vitaboreshwa zaidi. Pia inatarajiwa kuwa uwanja unaweza kuhudumia ndege 16 za aina ya ATR 72 katika muda wa saa 12 za kazi au kuwahudumia abiria 100 wanaoingia na kutoka kwa saa moja. Kwa maana nyingine, uwanja unaweza kuhudumia ndege moja kila baada ya saa moja na nusu. Huu ni upanuzi mkubwa sana. Mradi unakusudia pia kuweka umeme katika uwanja huo ili ndege ziweze kutua usiku pia. Hata hivyo, kuna uwezekano kuwa idadi ya abiria watakaohudumiwa uwanjani hapo ikashuka hadi 40 kwa saa, badala ya 100 kama ilivyopangwa hapo mwanzo. Mabadiliko haya hata hivyo hayataathiri mipango na michoro ya awali ya upanuzi wa uwanja huo.

Lengo la mradi ni kuboresha na kukuza shughuli za uchumi. Sekta zitakazoguswa moja kwa moja ni kilimo, utalii, ufugaji, mawasiliano na uvuvi. Kadhalika, mradi utagusa masuala ya kijamii kama elimu, afya na upatikanaji wa maji safi na salama.

Kisiwa cha Mafia kimekuwa kivutio kikuu cha utalii, kwa kuhudimia soko la kimataifa kwa kuunganisha watalii wanaokwenda Zanzibar na sehemu nyinginezo Tanzania bara. Idadi ya ndege, abiria na mizigo kwenda au kutoka Mafia imebadirika katika miaka ya hivi karibuni, ikiwa ni pamoja na kukua kwa biashara kati ya Mafia na sehemu nyingine. Kwa mfano, utuaji wa ndege umeongezeka kwa asilimia 30 kutoka ndege 1,290 mwaka 1999 kufikia ndege 2,146 mwaka 2007. Usafirishaji wa mizigo ulianza mwaka 2003 kwa mizigo yenye uzito kwa kilo 1,640 na kufikia kilo 11,615 kwa mwaka 2007. Abiria nao waliongezeka kutoka 6,609 mwaka 1999 na kufikia 13, 240 kwa mwaka 2007. Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania inakadiria ongezeko la abiria na mizigo kufikia kilo 318,084, abiria 40, 951 na safari za ndege karibu 6,567 katika kipindi cha miaka kumi ijayo. Idadi hii inaweza kuongezeka zaidi ya hapo ifikapo mwaka 2030 ambapo inakadiriwa

kutakuwepo na kilo milioni 1. 4 za mizigo na abiria karibuni 180,000.[1]

## MASUALA MUHIMU YA KUZINGATIWA

Kisiwa cha Mafia kina utajiri mkubwa wa bioanuai kama vile aina mbalimbali za samaki, pweza na ngisi. Uvuvi ni shughuli kuu ya kiuchumi kwa wakazi wa Mafia na maeneo jirani. Hata hivyo aina zote za samaki mbali na ngisi zimevuliwa kupita kiasi na sasa hivi hazipatikani kwa urahisi. Kisiwa cha Mafia pia kina utajiri wa wanyama pori kwa mfano aina za vyura na mijusi inayopatikana Mafia tu; popo wakubwa wanaoishi kwenye mapango. Rasilimali nyingie muhimu kwa Mafia ni ardhi, watu, maeneo ya kihistoria ambavyo vyote ni muhimu katika kukuza utalii.

Kuongezeka kwa idadi ya watalii Mafia kutaamsha mahitaji zaidi na kutoa fursa ya kujenga hoteli, vituo vya kupigia mbizi na huduma nyinginezo; hali itakayo sababisha kuongezeka kwa watu na utalii kisiwani Mafia. Kadhalika, ongezeko hili linaweza kuleta ukuaji wa shughuli za uchumi na kuboresha huduma za jamii. Kwa ujumla, matokeo ya kuongeza kwa shughuli za kiuchumi Mafia kutasababisha kuongezeka kwa mahitaji kama ardhi, maji, nishati, chakula, na kutazalisha taka ngumu na taka laini kwa wingi zaidi na kusababisha uharibifu wa mazingira au kuleta mabadiliko katika mila na destruri za wakazi wa Mafia.

Kwa sasa rasilimali za Mafia zipo hatarini kuharibika zaidi kutokana na mahitaji kuongezeka wakati usimamizi wa rasilimali hizo ni duni mno, umasikini unaongezeka na ruzuku kwa taasisi zinazo simamia rasilimali kuwa ndogo. Ni katika hali hii ndio maana Serikali ya Tanzania na Shirika la Changamoto za Milenia Tanzania waliamua kufanyika kwa Tathmini ya Mkakati ya Mazingira kwa Mafia ili kuona mambo ambayo yatahitaji uamuzi wa kisera. Lengo la tathmini hii ni kushauri mfumo wa upangaji na usimamizi wa Rasilimali za Mafia na kuanisha vipaumbele ambavyo serikali na Mradi wa Milenia watavifanyia kazi. Baadhi ya mabadiliko yatakayotokana na kuongezeka kwa shughuli za uchumi yataathiri utalii kwa ujumla. Yafuatayo ni mapendekezo ya kisera ambayo kama yakitekelezwa yatapunguza athari katika sekta ya utalii.

## MAPENDEKEZO YA KISERA

### 1. *KUPUNGUZA IDADI YA WAGENI KWA SIKU*

Hapo awali mradi wa uboreshaji wa uwanja wa ndege ulilenga kuhudumia abiria 100 kwa saa kwa abiria wanaoingia na kutoka Mafia. Huu ni wastani wa ndege 16 za ukubwa wa ART 72 kila baada ya ya saa moja na nusu katika muda wa kazi wa saa 12. Kufikia mwaka 2007, kiasi cha abiria 40 walikuwa wanafika Mafia kila siku (wastani wa abiria 13,240 kwa mwaka). Kuna vyumba 78 katika hoteli zilizopo sasa. Wakati idadi ya wageni wanaofika Mafia kwa siku ni ndogo kuliko idadi ya vyumba vilivyopo kwa sasa, Mafia hukabiliwa na upungufu wa vyumba hasa wakati wa msimu wa utalii, na zaidi upungufu huu hutokana na mipango duni ya kuweka vyumba.

Idadi ya wageni imepunguzwa kutoka 100 kwa saa hadi 40 kwa saa (wastani wa wageni 480 katika muda wa kazi wa saa 12) Idadi hii ya wageni ni sawa na ndege saba aina ATR 72 kwa siku au ndege moja kila baada ya saa moja na dakika saba.

Mbali ya mabadiliko haya, madhara ya idadi hii ya wageni katika mazingira ya Mafia bado ni makubwa. Ni muhimu kwa hiyo kuzingatia hoja ya kupunguza zaidi idadi ya wageni wataokuja Mafia kwa saa hata kufikia nusu ya idadi iliyopendekezwa. Izingatiwe kuwa kupunguza idadi ya wageni kwa saa kufikia nusu, kutaathiri matarajio ya mapato yatakayotokana na usafirishaji na hoteli kwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, wenye mahoteli, Mamlaka ya Mapato Tanzania na

[1] Makadirio haya yalifanywa kabla ya kutokea kwa tatizo la kuporomoka kwa uchumi duniani, ambapo inawezekana watalii watakaokuja Tanzania watapungua.

wenyeji wa Mafia kwa ujumla. Mafia bado iko nyuma kimaendeleo kwa hivyo si rahisi kupata wananchi wataounga mkono hoja hii, lakini kupitia njia mbalimbali, muafaka unaweza kupatikana. Suala hili linahitaji uamuzi wa kimkakati na kisera kwa kuwa linagusa ukusanyaji wa mapato, lakini ni muhimu kulizingatia kwa kutilia maanani faida zake katika uchumi na mazingira kwa muda mrefu, kuliko kufikiria faida za muda mfupi peke yake. Faida zaitakazotokana na matumizi bora ya mazingira zitakuwa za muda mrefu zaidi.

### 2. KUBORESH HOTELI ZILIZOPO SASA NA KUZUIA UJENZI WA HOTELI MPYA

Ili kupunguza madhara yatokanayo na kuongezeka kwa shughuli za ujenzi, uliosababishwa na ongezeko la watu Mafia, uamuzi wa kimkakati na kisera lazima ufanyike. Uamuzi huu ni wa kuzuia ujenzi wa hoteli mpya hadi zile zilizopo zimekarabatiwa na zimeanza kutoa huduma ya kimataifa. Wazo hili litekelezwe sanjari na pendekezo la kutayarisha mpango wa matumizi ya ardhi ambayo utaainisha maeneo na ukubwa wa hoteli tarajiwa.

Sasa hivi kuna mipango ya kujenga hoteli nyingine tano kwenye fukwe za Mafia. Mipango hii inaweza kusitishwa kwa muda wakati uongozi wa Mafia na Idara ya Utalii, Wizara ya Mali Asili na Utalii wanajipanga upya kukamilisha ramani za matumizi bora ya ardhi na mipango miji. Uamuzi huu wa serikali unaweza kuleta mgogogro miongoni mwa wawekezaji lakini serikali haina budi kuusimamia ili kunusuru mazingira ya Mafia.

### 3. KUANZISHA NA KUENDELEZA VIVUTIO VINGINE

Vivutio muhimu vya utalii kwa Mafia ni pamoja na kupiga mbizi, michezo ya baharini, uvuvi wa michezo, kusafiri na vyombo baharini na kutembelea vivutio vya utamaduni, historia na kuzuru msitu wa Mlola wenye viumbe mbalimbali. Japo kuwa vivutio vya baharini kwa Mafia ni vizuri kuliko sehemu nyingine Afrika Mashahriki, bado kumekuwepo na idadi ndogo ya wageni wanaotembelea maeneo hayo. Wageni katika hoteli wamekuwa wakifika kwa wastani wa asilimia 30 ya uwezo wa hoteli zote. Sababu kubwa ya hali hii ni kukosekana kwa usafiri wa uhakika kufika Mafia na kutokuwepo na vivutio zaidi vya kuwafaanya watlii wakae siku nyingi zaidi Mafia

Wizara ya Mali Asili na Utalii kwa kushirikiana na Bodi ya Utalii Tanzania, wamenza mchakato wa kuitangaza Mafia kama kivutio kikubwa. Lakini mchakato huu ni budi ukazingatia adhari za kuwa na wageni wengi Mafia wakati vivutio ni vile vile vichache.

### 4. KUKUZA UTALII KWA KUUNGAISHA SEKTA ZOTE ZINAZOCHANGIA KATIKA BIASHARA YA UTALII

Shughuli za utalii zimekuwa zikiendelea Mafia kwa takribani zaidi ya miaka 60 sasa. Pamoja na hali hiyo, bado utalii wa Mafia haujawanufaisha watu wenyeji wa huko. Hali hii inasababishwa na mipango mibovu ambayo haioianishi shughuli za utalii na sekta nyingine ambazo zinachangia katika utalii. Kwa mfano, utalii utafanikiwa tu mahali ambapo kuna chakula cha kutosha. Kwa hiyo, kama kuna mipango ya kupanua utalii paisipo kuhusisha sekta ya kilimo, utalli huo unakua hauna faida kwa watu wa kawaida. Hali hii imeikumba wilaya ya Mafia na sehemeu nyingine hapa Tanzania ambapo utalii unaonekana hauna uhusiano na sekta nyingine.

Serikali itunge "sera pendelezi" zitakazo wawezesha wananchi kujihusisha na biashara ya utalii moja kwa moja au kupitia uzalishaji wa mahitaji mbali mbali yanayohitajika katika mahoteli ya kitalii.

Pamoja na hilo, Halmashauri ya Wilaya pia ni lazima ianzishe programu za kuwawezesha wananchi kuzalisha bidhaa zinazotakiwa katika mahoteli. Kwa kufanya hivyo, sekta ya Utalii itapanuka sanjari na sekta nyingine na kuleta tija na faida kwa wananchi na serikali kwa ujumla.